

Bw. Dijon DaCosta, Sr., *Mwenyekiti wa Bodi*  
 Bi. Deirdre P. Pierce, *Makamu Mwenyekiti*  
 Bi. Anna Hill  
 Bi. Whitney McGinniss  
 Bi. Allyson Gevertz  
 Bi. Vickie B. Turner  
 Dk. Joyce Morley



Dk. Devon Q. Horton, *Msimamizi*

## INAPASWA KUCHAPISHWA BILA KUKAWIA

Jumane Ijumaa, 26 Julai 2024

## Mawasiliano:

Donald Porter, *Ed.D.* 678-481-4110  
 Carla Parker 404-734-1717

## DCSD Yatangaza Upanuzi wa Mpango wa Milo Isiyolipishwa kwa Shule 105

(STONE MOUNTAIN, GA) — Wanafunzi zaidi wa Wilaya ya Shule ya Kaunti ya DeKalb (DCSD) wataweza kupata kiamsha kinywa na chakula cha mchana bila malipo wakati wa mwaka wa masomo wa 2024-25! Wilaya ina furaha kutangaza kuwa mpango wa lishe wa Community Eligibility Provision (CEP) umepanuliwa. Mpango huu sasa unatolewa katika shule 105, na mwanafunzi yeyote anayehudhuria mojawapo ya shule za CEP atashihiki kupata kiamsha kinywa na chakula cha mchana bila malipo.

“Tuna furaha kupanua idadi ya shule kwenye mpango wa CEP katika Wilaya ya Shule ya Kaunti ya DeKalb kutoka 75 hadi 105,” alisema Dkt. Connie Walker, Mkurugenzi Mtendaji wa Huduma za Lishe ya Shule za DCSD. “Mpango inayosaidia wanafunzi na jamii ni muhimu kwa mafanikio ya kimasomo. Kama Huduma za Lishe ya Shule tutafanya tuwezavyo kwa uwezo wetu ili kuwasaidia wanafunzi kujiandaa kwa masomo kadiri iwezekanavyo.”

Mpango wa CEP huwezesha shule na wilaya katika maeneo yenye umaskini mkubwa kutoa kiamsha kinywa na chakula cha mchana bila gharama kwa wanafunzi wote waliojiandikisha bila kuhitaji maombi ya familia. Shule zinazotumia CEP hupewa fedha kwa kutumia fomula kulingana na asilimia ya wanafunzi wanaostahiki haswa kupata milo ya bila malipo kulingana na ushiriki wao katika mipango mingine mahususi iliyojaribiwa, kama vile Mpango wa Msaada wa Lishe ya Ziada (SNAP) na Msaada wa Muda kwa Familia zenye Mahitaji (TANF).

Ikiwa mwanafunzi wako hayupo kwenye orodha ya CEP, wanafunzi wanaweza kustahiki kupata [milo isiyolipishwa na iliyopunguzwa bei](#). Ili kuomba msaada wa milo, tembelea [www.schoolcafe.com](http://www.schoolcafe.com). Menu mpya ya vyakula ya DCSD kwa mwaka wa masomo wa 2024-25 inaweza kutazamwa katika <https://www.dekalbschoolsga.org/school-nutrition/menus/>.

XXX